European Journal of
Linguistics
(EJL)

# Usahihi wa Uhawilishaji wa Viwakilishi vya Jinsia katika Vitabu vya Kiingereza Vilivyotafsiriwa kutoka Kiswahili



# Usahihi wa Uhawilishaji wa Viwakilishi vya Jinsia katika Vitabu vya Kiingereza Vilivyotafsiriwa kutoka Kiswahili

[1*]**Mutisya Cosmas Mbithi,** [1]**Dr. Sarah Ndanu Ngesu,** [1]**Dr. Esther N. Chomba**

[1]South Eastern Kenya University

https://orcid.org/0009-0000-0260-5079

***Accepted:** 10th April 2025 Received in Revised Form: 9th May, 2025 Published: 12th June, 2025*

**IKISIRI**

**Kusudi:** Utafiti huu ulichunguza usahihi wa uhawilishaji wa viwakilishi vya jinsia katika vitabu vya Kiingereza vilivyotafsiriwa kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza. Utafiti huu ulidhamiria kuchunguza na kubainisha usahihi wa uhawilishaji wa viwakilishi vya jinsia kutoka kiswahili lugha isiyo na viwakilishi bainifu vya jinsia kwenda kiingereza lugha yenye viwakilishi bainifu ya jinsia.

**Mbinu:** Data za utafiti zilipatikana kwa kusoma, kuchanganua na kuhakiki tafsiri ya vitabu teule vya fasihi: *Siku Njema* ya Walibora (1996) na tafsiri yake *A Good Day* iliyotafsiriwa na Kweyu na Kawegere (2019), *Kaburi bila Msalaba* iliyoandikwa na Kareithi (1969) na tafsiri yake ya Kiingereza *Unmarked Grave* iliyotafsiriwa na Githiora (2017). Vilevile, mtafiti aliangazia tamthilia mbili; Tamthilia ya *Natala* iliyoandikwa na Mberia (1997) na tafsiri yake ya Kiingereza *Natala* iliyotafsiriwa na Kasu na Marami (2011). Tamthilia ya *Kinjekitile* iliyoandikwa na Hussein (1969) na tafsiri yake *Kinjekitile* iliyotafsiriwa na Hussein mwenyewe (1970) ilichunguzwa. Mtafiti aliteua vitabu hivi kwa kuwa vilionesha utajiri wa data inayohusu uhawilishaji wa viwakilishi vya jinsia. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya *Skopos* na Nadharia ya Usawa wa Kidhima. Nadharia ya *Skopos* iliyoasisiwa na Hanns Vermeer (1978) ambayo husisitiza kuwa, kimsingi kutafsiri kunafaa kushughulikia jukumu la matini chanzi na matini lengwa yaani tafsiri ni kitendo chenye malengo. Nadharia ya Usawa wa Kidhima iliasisiwa na Nida (1964) na inatilia mkazo usawa wa kimaana na athari sawa kwa hadhira katika mchakato wa tafsiri. Baada ya kubainisha uhawilishaji wa viwakilishi vya jinsia, data hiyo ilichanganuliwa kitaamuli na kitakwimu na matokeo kuwasilishwa kupita maandishi ya kinadhari majedwali na michoro ya miche duara kutathimini usahihi uhawilishaji huo.

**Matokeo:** Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa wafasiri wa vitabu teule wamehawilisha viwakilishi vya jinsia kwa usahihi na uhawilishaji mwingine ukazua utata. Uhawilishaji wa viwakilishi vya jinsia unachangamoto nyingi kwa hivyo wafasiri wanapaswa kumakinika kwani, uhawilishaji wa viwakilishi vya jinsia huwa na athari asi na chanya kwa hadhira lengwa.
**Mchango wa kipekee kwa nadharia, vitendo na sera:** Utafiti huu unapendekeza utafiti zaidi kufanywa katika uhawilishaji wa viwakilishi vya nyakati katika tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza kwani kama uhawilishaji wa viwakilishi vya jinsia, uhawilishaji wa viwakilishi vya wakati vilevile, vinaweza kuwa na athari kwa ujumbe asilia.

**Maneno ya kimsingi:** *Viwakilishi vya kijinsia, Usahihi wa uhawilishaji, Tafsiri, Lugha lengwa, Hadharia lengwa.*

European Journal of Linguistics
ISSN: 2957-4641 (online)
Vol. 4, Issue No. 2, pp 1 - 17, 2025 www.carijournals.org

**Utangulizi**

Tafsiri ni njia moja ya kuhamisha ujumbe na maarifa kutoka lugha moja hadi nyingine. Tafsiri nyingi zinazohusisha fasihi ya Kiswahili zimeegemea katika tafsiri kutoka lugha ya Kiingereza kwenda Kiswahili. Hata hivyo, kwa mujibu wa Kimutai (2016) na Ngesu na Wenzie (2019), kuna mwamko mpya wa kutafsiri kazi za Kiswahili kwenda Kiingereza na lugha nyinginezo. Utafiti huu ulikuwa na lengo la kudadisi usahihi wa uhawilishaji wa viwakilishi vya jinsia katika vitabu vya Kiingereza vilivyotafsiriwa kutoka Kiswahili. Kazi za fasihi zilizoshughulikiwa ni pamoja na riwaya mbili ambazo ni; *Kaburi Bila Msalaba* iliyoandikwa na Kareithi (1969) na tafisiri yake *Unmarked Grave* iliyofanywa na Githiora (2017) na *Siku Njema* ya Walibora (1996) na tafsiri yake *A Good Day* iliyofanywa na Kweyu na Kawegere (2019). Aidha, tamthilia mbili zilishughulikiwa zikiwa ni; *Natala* ya Mberia (1997) na tafsiri yake *Natala* iliyofanywa na Kasu na Marami (2011) na *Kinjeketile* yake Hussein (1969) na tafsiri yake *Kinjeketile* iliyotafsiriwa na Hussein Mwenyewe (1970).

Akiangazia Nadharia ya *Skopos*, Vermer (1978), anasema kuwa, matini lengwa lazima iibue maana inayoeleweka na hadhira lengwa na katika muktadha wa kimawasiliano. Hata hivyo, ilibainika kupitia mapitio ya vitabu vilivyotafsiriwa kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza kuwa baadhi ya tafsiri huwa sahihi huku tafsiri nyingine zikiwa tenge. Hivyo basi, utafiti huu ulilenga kudadisi na kubainisha usahihi wa uhawilishaji wa viwakilishi vya jinsia katika tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza.

**Msingi wa Nadharia**

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya *Skopos* na Nadharia ya Usawa wa Kidhima. Mtazamo wa *Skopos* uliasisiwa na mfasiri wa kijerumani Hans Vermeer (1978). Mchakato wa tafsiri huamuliwa na utendakazi wa kazi iliyotafsiriwa (Munday, 2001). Neno '*skopos'* ni la Kigiriki linalomaanisha lengo kuu la kufanya shughuli ya tafsiri. Kwa mujibu wa nadharia hii, kutafsiri ni kutoa matini lengwa ambayo ina jukumu linalofaa kama ilivyo katika matini chanzi. Nadharia hii husisitiza kuwa, kimsingi kutafsiri kunafaa kushughulikia jukumu la matini chanzi na matini lengwa. *Skopos* hutazama kutafsiri kama kitendo chenye malengo (Halliday, 2000). Kitendo hicho kinastahili kumlenga mpokeaji kwenye mazingira ya tafsiri hiyo.

Kulingana na nadharia hii, kutafsiri ni kuzalisha matini lengwa, kwa lengo lengwa na mpokezi lengwa katika mazingara lengwa (Schaffner, 1998). Kwa hivyo, kufuatia lengo la utafiti huu nadharia hii ilisaidia kuchunguza kama wafasiri wa kazi teule za fasihi zilizotafsiriwa kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza wamezalisha upya matini lengwa ikimlenga mpokeaji pamoja na ujumbe asilia kwenye matini chanzi hasa wanapohawilisha viwakilishi vya jinsia.

Nadharia ya Usawe wa Kidhima iliasisiwa na Nida (1964). Kulingana na Nida, lengo mahususi la Nadharia hii ni kujaribu kupunguza tofauti zilizopo kati ya utamaduni na isimu katika tafsiri. Aidha, kwa kuzingatia Nadharia hii tafsiri inafaa kutumia lugha rahisi inayoeleweka na waliokusudiwa. Vilevile, tafsiri inafaa kuwa bora kiasi kuwa msomaji asiweze kugundua kuwa kazi anayoisoma imetafsiriwa.

Akiendeleza Nadharia hii, Venuti (2000) anaongeza kuwa Nadharia ya Usawe wa Kidhima

humruhusu mfasiri kubadilisha lugha, nahau, misimu, usemi, na semi za tanakali za sauti kulingana na utamaduni wa lugha lengwa. Pia, inamtaka mfasiri azingatie semi za kisasa kwa sababu semi za kileksia hubadilika kiwakati. Venuti (2000) anafafanua kauli ya Nida kwa kuongeza kuwa tafsiri inaweza kuwa makadirio, kwa sababu hakuna lugha mbili zinazofanana moja kwa moja. Kwa hivyo, athari ya jumla ya tafsiri inaweza kuwa karibu na ya asili, lakini hakuwezi kuwa na ufanano wa moja kwa moja.

## Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ulifanyika maktabani ambapo ulihusisha kusoma vitabu teule na kuvichambua kwani, kwa mujibu wa Riazi (2018) na Khan (2019), uchambuzi wa nyaraka ni mbinu inayotumiwa kukusanya data na taarifa kutoka kwenye maandishi mbalimbali ambayo yamechapishwa au ambayo hayajachapishwa. Katika utafiti huu, matini za Kiswahili na Kiingereza zilisomwa kwa kina, yaani, *Siku Njema*, *Kaburi bila Msalaba*, *Natala* na *Kinjeketile* kwa kuvilinganisha na tafsiri zake; *A Good Day*, *An Unmarked Grave*, *Natala* na *Kinjeketile*. Pia, utafiti wa maktabani ulihusu kusoma tasnifu, majarida na makala mengineyo ili kupata taarifa zinazohusiana na lengo la utafiti huu.

Vitabu hivi viliteuliwa kimakusudi baada ya kusoma riwaya na tamthilia nyinginezo na kubaini kuwa vitabu vilivyoteuliwa vilikuwa na utajiri wa viwakilishi vya jinsia na vingetoa data faafu kwa utafiti. Utanzu wa Hadithi fupi haukuangaziwa kwani ukilinganishwa na utanzu wa riwaya kwa kuagazia vipengele kama; maudhui, wahusika miongoni vipengele vingine vilikuzwa kwa undani zaidi katika riwaya kuliko hadithi fupi kwa hivyo uwawilishaji wa viwakilishi vya jinsia ulikuwa wa kina katika riwaya. Vilevile, utanzu wa ushairi haukushughulikiwa kwa kuwa moja wapo wa vitabu teule *Siku Njema* kuna mashairi kwa hivyo uhawilishaji wa viwakilishi vya jinsia katika ushairi ulishughulikiwa. Data ilichanganuliwa kitaamuli na kitakwimu na matokeo kuwasilishwa kupitia maandishi ya kinadhari, majedwali na michoro ya michi duara.

## Matokeo ya Utafiti

Baada ya kusoma na kubainisha uhawilishaji wa viwakilishi vya jinsia katika vitabu teule, mtafiti alichanganua data na kuhakiki usahili wa uhawilishaji wa viwakilishi vya jinsia katika vitabu teule ili kusaidia kutimiza lengo la utafiti.

### Riwaya ya *Kaburi bila Msalaba* na Tafsiri yake *Unmarked Grave*

Mfasiri amehawilisha viambishi viwakilishi vya jinsia kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa katika mchakato wa tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza. Jedwali Na. 1 linaonesha uhawilishaji huo.

**Jedwali Na. 1: Tathmini ya usahili wa uhawilishaji wa viambishi viwakilishi vya jinsia katika *Kaburi bila Msalaba***

| Na. | Kipashio cha Kiswahili | Tafsiri ya Kiingereza |
|---|---|---|
| 1. | *A*liwataja wote … (uk. 3) | *She* had revealed the names (uk. 3) |
| 2. | Askari mwingine ali*mw*ambia (uk. 11) | Another askari ordered *her* (uk. 10) |
| 3. | *A*liketi akapiga goti (uk. 11) | *He* knet on his right knee … (uk. 11) |
| 4. | Yule mtu *a*li*m*tazama tu bila kufunga macho (uk. 12) | The man stared at *her* without blinking … (uk. 11) |
| 5. | Meja blue *ha*kuwa na … (uk. 16) | *He* didn't have a … (uk. 14) |

**Chanzo: Data ya maktabani (2025)**

Mfano katika Jedwali Na. 1 unaonesha kuwa kiambishi *"a"* kimetafsiriwa na kuwa *"she"* katika Kiingereza kiwakilishi cha jinsia ya kike. Vilevile, kiambishi *"-m-"* kimetafsiriwa na kiwakilishi cha jinsia ya kike "*her"* kikatumika katika lugha lengwa (Kiingereza). Viambishi hivi vinatenganisha Nyaguthii ambaye anatajwa tu na mhusika Mumbi lakini jinsia yake haijabainika hivyo, katika tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza, viwakilishi vya jinsia "*she*" na "*her*" vimehawilishwa, na haibainiki mfasiri alitumia vigezo vipi kutambua kwamba, jinsia ya Nyaguthii ilikuwa ya kike. Labda, huenda mfasiri alichukulia kwamba Mumbi alikuwa mwanamke, na Nyaguthii alikuwa rafikiye, huenda mtazamo huo ulimwongoza mfasiri kutoa jinsia ya mhusika huyo kuwa ya kike; vilevile, huenda mfasiri alikuwa anafahamu majina kutokana na uelewa wake wa makabila ya nchi husika ndio maana akasema Nyaguthii ni mwanamke lakini kutokana na utangamano wa wanajamii, hata Nyaguthii anaweza kuwa wa kabila tofauti kama vile, mkamba mwanamme aliyepewa jina hilo. Kauli hii inaungwa mkono na Guilleman na Grosjean (2001) wanapodai kuwa, lugha nyingi hugawa uhusiano wa makundi ya nomino kijinsia kwa kuangazia vipengele kama hadhi, umbo, mahusiano na kadhalika.

Isitoshe, katika mfano Na. (2), kiambishi *"-mw-"* katika kitenzi, "ali*mw*ambia", kinarejelea mhusika Mumbi ambaye ndiye anayewakilishwa na kiwakilishi cha jinsia ya kike "*her*" katika tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza. Aidha, katika mfano huo huo wa (2) kiambishi *"-m- "* kimetumika katika kitenzi "a*m*letee" kuwakilisha askari katika lugha lengwa. Uhawilishaji huu ni tenge kwa kuwa jinsia ya askari haikuwa wazi katika lugha chanzi. Huenda mfasiri alichukulia kuwa utamaduni wa waafrika na hasa jamii ya wanakaburi bila msalaba, askari huwa wanaume au kazi ya askari ni ya wanaume, lakini uhalisia, unabaini kuwa askari huwa wa jinsia zote kike na kiume. Kama anavyodai Buljan na wenzake (2013) kuwa viwakilishi ya jinsia kisarufi huwakilisha jinsia zote kike na kiume.

Aidha, kutokana na mfano Na. (4) kiambishi *"-m-"* katika kitenzi "ali*m*tazama" kimetafsiriwa na kiwakilishi cha jinsia ya kike "*her*" kikahawilishwa katika "stared at *her*…" uhawilishaji huu ni sahihi kwa kuwa anayewakilishwa na kiwakilishi "*her*" ni mhusika Mumbi na jinsia

yake imetambuliwa katika lugha lengwa kuwa ya kike. Mfano Na. (5), unabainisha kuwa, kiambishi "*ha*-" kimehawilishwa na kiwakilishi cha jinsia ya kiume "*he*" kikatumika katika sentensi:

"Meja blue *ha*kuwa na …" - "*he* didn't have …".

Uhawilishaji huu ni sahihi kwani katika lugha chanzi, mhusika anayezungumziwa (*meja blue*) alitambulishwa, kama, "*Kijana* mmoja … aliongoza …". Japo neno "*kijana"* katika lugha ya Kiswahili hutumika kurejelea jinsia zote kiume na kike, huenda maelezo zaidi yanayotolewa katika mfano (5) "hakuwa na *bibi* …" yalimwongoza mfasiri kutoa jinsia ya *meja blue* kwani kulingana na muktadha na utamaduni wa kiafrika, ni mwanamme tu anayeweza kusemekana "hakuwa na *bibi*…". Lakini, mabadiliko mapya yameibuka kuhusu asasi ya ndoa ambapo jinsia zote kike na kiume zinaoana. Aidha, mfasiri amehawilisha maneno kamili katika lugha chanzi na kuyawakilisha katika lugha lengwa kwa kutumia viwakilishi vya jinsia katika tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza. Hata hivyo, mfasiri alihawilisha maneno kamili kwa misingi ya kijinsia. Jedwali Na. 2 linaonesha tathmini ya uhawilishaji huo.

**Jedwali Na. 2: Tathmini ya usahihi wa uhawilishaji wa viwakilishi (maneno) vya jinsia katika *Kaburi bila Msalaba***

| **Na.** | **Kipashio cha Kiswahili** | **Tafsiri ya Kiingereza** |
|---|---|---|
| **1.** | Chifu hakuweza kujua kwa nini *msichana* mzuri kama … (uk. 4) | The chief could not understand why such beautiful *woman* … (uk. 4) |
| **2.** | Pamoja na Mumbi palikuwepo na *wazee* wengine wawili na *kijana* mmoja (uk. 9) | In addition to Mumbi there were other two elderly *men* and *a young man* |
| **3.** | Watu wengi, *watoto wanaume* na *wanawake* (uk. 10) | Many *young men* and *women* |
| **4.** | Akaona *mtu* … kama ya mnyama (uk. 11) | Animal-like eyes of a *man* … (uk. 10) |
| **5.** | Kikundi cha *askari polisi* kutoka … (uk. 12) | A group of *policemen* from … (uk. 11) |
| **6.** | … *mke wake* … (uk. 12) | … *his wife* … (uk. 11) |
| **7.** | *Mjaluo* mmoja kwa jina … (uk. 13) | A *Luo man* named … (uk. 12) |

**Chanzo: Data ya maktabani (2025)**

Kiwakilishi cha jinsia ya kike katika lugha chanzi *"…msichana*" kwenye mfano Na. 1 kimehawilishwa na kuwakilishwa na kiwakilishi "*woman*" katika lugha lengwa. Uhawilishaji huu unabainisha jinsia ya mhusika Mumbi anayewakilishwa katika lugha chanzi lakini kwa uchunguzi zaidi mfasiri alitumia kiwakilishi "*woman*" badala ya "*girl*" kwa mujibu wa muktadha wa lugha chanzi. Vilevile, katika mfano Na. (2), maneno "*wazee*" na "*kijana*" yametafsiriwa na kuwa "*men*" na "*a young man*" mtawalia. Maneno "*wazee*" na "*kijana*" kwa lugha ya Kiswahili mara nyingi hutumiwa kurejelea jinsia zote mbili ya kike na kiume, lakini

mfasiri alichagua jinsia ya kiume kwa kutumia neno "*men*" na "*young man*" kama viwakilishi katika tafsiri katika Kiswahili kwenda Kiingereza.

Katika mfano Na. (3) maneno "*watoto*", "*wanaume*" na "*wanawake*" yamehawilishwa na kuwa na kuwa "*young men*" na "*women*" mtawalia katika tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza. Uhawilishaji huu ni sahihi kwa kuwa wahusika wanaorejelewa katika lugha chanzi na kuwakilishwa katika lugha lengwa jinsia zao zimebainishwa. Aidha, katika mfano Na. (4), neno "*mtu*" limehawilishwa na kuwa "*man*".

"Akaona *mtu* amemkondolea macho …" "…animal-like eyes of a *man* …"

Matumizi ya kiwakilishi "*man*" katika tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza unakuwa tenge kwa kuwa, mhusika Mumbi anasema tu, aliona macho ya mtu wala hajasema ni mwanamke au mwanaume katika lugha chanzi.

Kutokana na mfano Na. (5), "… *kikundi cha askari polisi* …"- "… *A group of policemen* …" mfasiri amehawilisha na kutumia kiwakilishi cha jinsia ya kiume "*men*" katika lugha lengwa katika tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza. Uhawilishaji huu unatoa jinsia ya askari polisi kuwa ya kiume, jambo ambalo si wazi katika lugha chanzi. Huenda mfasiri alichukulia kuwa, kazi ya askari ni ya jinsia ya kiume au utamaduni na muktadha wa riwaya ulitoa mwongozo wa askari wote kuwa kiume.

**Riwaya ya *Siku Njema* na tafsiri yake *A Good Day***

Mfasiri vilevile, alihawilisha viwakilishi vya jinsia katika riwaya teule *Siku Njema* kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza. Jedwali na. 3 linaonesha tathmini ya usahili wa uhawilishaji huo

**Jedwali Na. 3: Tathmini ya usahihi wa uhawilishaji wa viambishi viwakilishi vya jinsia katika *Siku Njema***

| **Na.** | **Kipashio cha Kiswahili** | **Tafsiri ya Kiingereza** |
|---|---|---|
| 1. | *A*likuwa kitindamimba … (uk. 1) | *She* was the last born … (pg. 1) |
| 2. | Zawadi *a*lifungua moyo … (uk. 85) | Zawadi opened *her* heart … (pg. 88) |
| 3. | *A*fichaye uchi hazai … (uk. 94) | One who hides *her* nakedness cannot give birth (pg. 98) |
| 4. | *A*likuwa katambaliwa … (uk. 1) | Age had crept on *him* … (pg. 1) |
| 5. | *A*likuwa na karakana yake ya kutengeneza majeneza … (uk. 5) | *He* made coffins … (pg. 5) |
| 6. | ... *tu*andamane … (uk. 96) | … accompany *her* (pg. 101) |
| 7. | *Li*kanilazimisha kutenda … (uk. 56) | *He* forced me to do … (pg. 59) |
| 8. | Ungali*mw*ita fremu au gofu la mtu (uk. 12) | *She* was a skeleton (pg. 12) |
| 9. | … nika*mw*ambia (uk. 24) | … I told *him* (pg. 24) |

**Chanzo: Data ya maktabani (2025)**

Uhawilishaji wa kiambishi kiwakilishi *"a"* katika mfano Na. (1) hadi (3), na katumia, viwakilishi vya jinsia ya kike, *"she"* na *"her"* katika tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza ni sahihi kwani wahusika wanaozungumziwa, jinsia zao zimebainishwa katika lugha chanzi. Kwa mfano katika mfano Na. (1) kiwakilishi *"a"* katika "*a*likuwa kitinda mimba …" kinawakilisha mhusika Zainabu, mamake Kongowea ambaye jinsia yake ni wazi katika lugha chanzi. Vilevile, mhusika zawadi amebainishwa kuwa mwanamke hivyo, matumizi ya viwakilishi *"she"* na *"her"* katika lugha lengwa na mfasiri ni sahihi.

Aidha, kiwakilishi hicho hicho *"a"* katika mfano Na. (4) na (5), vimehawilishwa na mfasiri akatumia viwakilishi vya jinsia ya kike, *"she"* na *"her"* na kiume *"him"* na *"he"* katika tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza. Uhawilishaji huu ni sahihi kwa kuwa anayezungumziwa ni babuye Kongowea ambaye asemekana "*a*likuwa katabaliwa …" na mfasiri akawakilisha mhusika huyu kwa kutumia kiwakilishi cha jinsia ya kiume "*him"* katika lugha lengwa na vilevile *"he"* kuwakilisha mhusika mjomba Kitwana katika tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza.

Isitoshe, katika mfano Na. (6), mfasiri amehawilisha kiwakilishi cha jinsia ya kike *"her"* kutokana na kiambishi kiwakilishi cha jinsia *"a"* katika lugha chanzi. Uhawilishaji huu ni tenge kwani, mfasiri anapotumia kitenzi "tu*a*ndamane …" haitoi jinsia ya mhusika anayerejelewa lakini anaposema "*accompany her*" badala ya "*we go together*" muktadha unatumika kutoa jinsia ya mhusika rejelewa. Vilevile, kiambishi kiwakilishi cha jinsia *"li-"* katika mfano Na. (7), mfasiri ametumia kiwakilishi cha jinsia ya kiume *"he"* uhawilishaji huu ni tenge kwa kuwa jitu halijatajwa ni la jinsia gani katika lugha chanzi huenda mfasiri aliongozwa na mtazamo kuwa, anayeweza kubaka mtu ni jinsia ya kiume na aliyekuwa anazungumziwa ni mwanamke japo hata jinsia badala ya kike, yaweza kuwa yarejelewa kwa kuwa pia, laweza lazimishwa kutenda jambo hilo kulingana na muktadha. Isitoshe, mfasiri alihawilisha maneno kamili kwa misingi ya kijinsia katika kutafsiri riwaya ya *Siku Njema* kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza. Jedwali Na. 4 linaonesha tathmini ya uhawilishaji huo.

***Jedwali Na. 4: Tathmini ya usahihi wa uhawilishaji wa viwakilishi (maneno) vya jinsia katika Siku Njema***

| Mfano | Kipashio cha Kiswahili | Tafsiri ya Kiingereza |
|---|---|---|
| 1. | *Mama* alinipa jina la Msanifu Kombo (uk. 3) | My *mother* ... Msanifu Kombo (pg. 3) |
| 2. | *Bibi yangu* alikuwa keshakufa wakati (uk. 3) | *My grandmother* had died by then (pg. 3) |
| 3. | *Mkaza mjomba* … (uk. 10) | *His wife* … (pg. 10) |
| 4. | *Mjomba* Kitwana alimsaidia … (uk. 10) | *Uncle* Kitwana helped her … (pg. 10) |
| 5. | *Mwa…naa…ngu* (uk. 13) | "*My ... so ... n* (pg. 13) |
| 6. | … *mwanangu* … (uk. 31) | … *my son* … (pg. 31) |
| 7. | … aliwaamuru *vigoli wawili* … (uk. 20) | … commanded *two young girls* … (pg.20) |
| 8. | Alikuwa *msichana* adibu na …(uk.20) | *She* was ... mannered and kind (pg. 20) |
| 9. | … *msichana* mmoja suriama … (uk. 105) | … half caste *girl* … (pg. 111) |
| 10. | *Mpwa wake* toka Tabora … (uk. 23) | … *her nephew* from Tabora (pg. 23) |

European Journal of Linguistics
ISSN: 2957-4641 (online)
Vol. 4, Issue No. 2, pp 1 - 17, 2025 www.carijournals.org

**Chanzo: Data ya maktabani (2025)**

Katika mfano Na. (1), mfasiri ametumia kiwakilishi cha jinsia ya kike *"mother"* katika lugha lengwa kuwakilisha kiwakilishi *"mama"* katika lugha chanzi. Matumizi ya kiwakilishi *"mother"* katika tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza ni sahihi kwani kisawe cha neno "*mama"* katika lugha ya Kiingereza huwa *"mother"*. Aidha, katika mfano Na. (2), mfasiri amehawilisha, kiwakilishi "*bibi"* katika lugha chanzi na kutumia kiwakilishi *"grandmother"* katika lugha lengwa. Uhawilishaji huu ni tenge kwani neno *"bibi"* laweza kumaanisha mke wa mtu au nyanya. Lakini kwa mujibu wa muktadha, anayerejelewa ni nyanyake Kongowea hivyo, mfasiri anapotumia kiwakilishi cha jinsia ya kike *"grandmother"* katika lugha lengwa ni sahihi. Katika mfano Na. (3), matumizi ya kiwakilishi cha jinsia ya kiume "*his wife"* yamejitokeza katika lugha lengwa kutokana na mhusika "*mkaza mjomba"* katika lugha chanzi.

"*mkaza mjomba …*" "*His wife …*"

Uhawilishaji huu ni sahihi kwani anayewakilishwa na viwakilishi *"his wife"* katika tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza ni mke wa mjombake Kongowea.

Aidha, katika mfano Na. (4), kiwakilishi *"uncle"* kimetumiwa na mfasiri katika lugha lengwa kutokana na kiwakilishi *"mjomba"* katika lugha chanzi.

"*Mjomba* Kitwana alisaidia …" "*Uncle* Kitwana helped …"

Matumizi ya kiwakilishi cha jinsia ya kiume *"uncle"* katika lugha lengwa ni sahihi kwani neno "*mjomba"* maana yake kwa Kiingereza ni *"uncle"* ndugu wa kiume wa mama mzazi. Mfano Na. (5) na (6) unabainisha matumizi ya kiwakilishi *"son"* katika lugha lengwa kutokana na kiwakilishi "*mwanangu"* katika lugha chanzi. Uhawilishaji huu ni sahihi kwani anayezungumziwa kulingana na muktadha ni Kongowea na jinsia yake ni ya kiume japo neno *"mwanangu"* laweza kuwakilisha jinsia zote kike na kiume.

**Tathmini ya usahihi wa uhawilishaji wa viwakilishi vya jinsia katika Tamthilia ya *Natala* na tafsiri yake ya Kiingereza *Natala***

Katika mchakato wa tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza viambishi viwakilishi vya jinsia vimehawilishwa kutoka lugha chanzi na mfasiri akaviwakilisha kwa kutumia viwakilishi vya jinsia katika lugha lengwa. Katika tamthilia ya *Natala* na tafsiri yake ya Kiingereza *Natala*. Jedwali na. 5 linaonesha uhawilishaji huo.

European Journal of Linguistics
ISSN: 2957-4641 (online)
Vol. 4, Issue No. 2, pp 1 - 17, 2025 www.carijournals.org

**Jedwali Na. 5: Tathmini ya usahihi wa uhawilishaji wa viambishi viwakilishi vya jinsia katika Tamthilia ya *Natala***

| Na. | Kipashio cha Kiswahili | Tafsiri ya Kiingereza |
|---|---|---|
| **1.** | *A*nachukua nguo moja wapo … (uk. 1) | *She* picks a piece of cloth … (pg. 1) |
| **2.** | *A*kichukua funguo kutoka mezani … (uk. 9) | Picking up *her* bunch of keys … (pg. 10) |
| **3.** | *A*nafunua jalada (uk. 9) | *He* opens up a folder that … (pg. 10) |
| **4.** | *A*nabadilika ghafla (uk. 19) | Abruptly *his* mien reverted … (pg. 21) |
| **5.** | *Ha*kupewa barua ni mimi niliyepewa (uk. 5) | I was the one who was given the letter not *him* (pg. 6) |
| **6.** | Pengine *ha*takunywa kesho … (uk. 7) | *He* might not be drunk tomorrow (pg. 8) |
| **7.** | *Ha*takaa sana … (uk. 14) | *She* won't be long (pg. 16) |
| **8.** | Aki*ji*pigapiga kifuani … (uk. 12) | Thumping *his* chest … (pg. 14) |
| **9.** | Ana*ji*funika uso kwa viganja (uk. 23) | Covering *her* face with *her* hands (pg. 25) |
| **10.** | *N*anyang'anywa shamba … (uk. 75) | *He* wants to grab my farm (pg. 81) |

**Chanzo: Data ya maktabani (2025)**

Kiambishi *"a"* katika mfano Na. (1) kimetafsiriwa na kuwa *"She"* katika lugha lengwa. Kiwakilishi "*she"* katika lugha ya Kiingereza huwakilisha jinsia ya kike. Katika lugha chanzi kiambishi *"a"* katika mfano "*a*nachukua nguo …" kinawakilisha Natala ambaye kesha tangulizwa ni mwanamke kwa hivyo, uhawilishaji *"a"* katika lugha chanzi na kuwa *"she"* katika lugha lengwa ni sahihi. Vilevile, katika mfano Na. (3) na (4) mfasiri ametumia viwakilishi vya jinsia ya kiume *"her"* na *"his"* katika tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza. Uhawilishaji huu umetokana na kiwakilishi *"a"* katika lugha chanzi. Uhawilishaji huu ni tenge kwa kuwa kiwakilishi *"a"* katika lugha chanzi kinawakilisha chifu na mwandishi hajabainisha jinsia ya chifu kuwa ya kike au kiume katika lugha chanzi.

Aidha, katika mfano Na. (3) kiambishi *"ha-"* kimetafsiriwa na kuwa *"him"* katika lugha ya Kiingereza na kawaida kiwakilishi *"him"* huwakilisha jinsia ya kiume katika lugha chanzi. Kwa mfano; "*ha*kupewa barua na mimi …" "I did give *him*…". Kiwakilishi "*ha*-" kinarejelea bwana ambaye amebainishwa ni mwanaume hivyo matumizi ya kiwakilishi *"him"* katika tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza ni sahihi. Vilevile, katika mfano Na. (6) kiambishi, "*ha*takunywa kesho …" – "he won't drink…" kiambishi *"ha-"* kimetafsiriwa na kuwa *"he"*

katika lugha chanzi. Kiwakilishi hiki kinawakilisha Wakene ambaye ni nduguye Tango. Kwa hivyo uhawilishaji huu ni sahihi.

Isitoshe, katika mfano Na. (7), kiambishi kiwakilishi *"-ji-"* katika fungu; kiambishi kiwakilishi "*-ji-*" kimehawilishwa na kiwakilishi cha nafsi ya kiume *"his"* kikatumiwa na mfasiri katika tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza. Uhawilishaji huu ni sahihi kwa kuwa kiwakilishi *"his"* katika lugha lengwa kinawakilisha Wakene katika lugha chanzi ambaye ni mwanamme kulingana na muktadha wa lugha chanzi. Hata hivyo, kiwakilishi hicho hicho *"-ji"*- katika mfano Na. (8), kimewakilishwa na kiwakilishi cha jinsia ya kike *"her"* katika tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza.

"Ana*ji*funika uso kwa viganja …"

"Covering *her* face with *her* hands …"

Uhawilishaji huu ni sahihi kwa kuwa anayerejelewa ni Natala na jinsia yake ya kike imebainishwa katika lugha chanzi. Zaidi ya hayo, mfasiri alihawilisha maneno kamili kwa misingi ya kijinsia. Jedwali na. 6 linaonesha uhawilishaji huo

***Jedwali Na. 6: Tathmini ya usahihi wa uhawilishaji wa viwakilishi (maneno) vya jinsia katika Natala***

| Na. | Kipashio Cha Kiswahili | Tafsiri Ya Kiingereza |
|---|---|---|
| **1.** | Nadhani yuko *kwake* … (uk. 8) | He must be in *his house* … (pg. 9) |
| **2.** | Hata *yeye* alianguka … (uk. 14) | *She* too felugha lengwa down (pg. 15) |
| **3.** | … kutoka kwa *kakangu* … (uk. 19) | … from my late *brother* … (pg. 21) |
| **4.** | Umkubali huyu *mwanao* … (uk. 27) | … receive this our *brother* (pg. 30) |
| **5.** | Singependa kuuona uso *wake* (uk. 27) | I can't bear to view *his* disfigured (pg. 31) |
| **6.** | Ni muhimu *kwake* na … (uk. 28) | It is important for *him* and … (pg. 31) |
| **7.** | Naheshimu hisia *zake* (uk. 28) | I respect *her* feeling (pg. 31) |
| **8.** | Mungu mpokee *mwanao* (uk. 28) | God receive your *son* (pg. 32) |
| **9.** | … asizikwe mpaka *yeye* … (uk. 28) | … shouldn't proceed until *he* arrives (pg. 32) |
| **10.** | … *mjane* na *watoto* (uk. 53) | … *a widow* and *his children* (pg. 57) |

**Chanzo: Data ya maktabani (2025)**

Katika mfano Na. (1), kiwakilishi cha jinsia "*kwake"* katika lugha chanzi kimehawilishwa na kuwakilishwa na kiwakilishi cha jinsia ya kiume *"his"* katika lugha lengwa.

"Nadhani yuko *kwake* …" "He must be in *his* house …"

Uhawilishaji huu ni sahihi kwa kuwa kiwakilishi *"his"* katika lugha lengwa kinawakilisha "*baba"* katika lugha chanzi na jinsia yake ya kiume imebainishwa katika muktadha wa lugha chanzi. Vilevile, kivumishi kiwakilishi cha nafsi *"yeye"* katika mfano Na. (2), kimehawilishwa na mfasiri akatumia kiwakilishi cha jinsia ya kike *"she"* katika tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza.

"Hata *'yeye'* alianguka …" "*She* too fell down …"

Uhawilishaji huu ni sahihi kwa kuwa anayerejelewa ni Alika na ametambulishwa kama mtoto ambaye jinsia yake ni ya kike.

Aidha, mfasiri katika mfano Na. (3) na (4) amehawilisha viwakilishi viwili tofauti katika lugha chanzi *"kakangu"* na *"mwanao"* na kuviwakilisha katika lugha lengwa kwa kutumia kiwakilishi kimoja cha jinsia ya kiume *"brother"*. Uhawilishaji huu ni sahihi kwa kuwa kiwakilishi *"brother"* katika lugha lengwa kinawakilisha viwakilishi *"mwanao"* na *"kakangu"* katika lugha chanzi na anayerejelewa kulingana na muktadha ni Tango ambaye ni mwanamme na kiwakilishi *"brother"* ni cha jinsia ya kiume. Hata hivyo, kiwakilishi *"mwanao"* katika lugha chanzi kwa mujibu wa mfano Na. (8), kimehawilishwa na mfasiri kutumia kiwakilishi cha jinsia ya kiume *"son"* katika tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza. Matumizi ya kiwakilishi cha jinsia ya kiume *"son"* katika lugha lengwa ni sahihi kwa kuwa anayerejelewa ni Tango na jinsia yake ni ya kiume.

**Tamthilia ya *Kinjeketile* na tafsiri yake *Kinjeketile***

Uhawilishaji wa viambishi viwakilishi ya jinsia kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza umebainika katika tafsiri ya *Kinjeketile* kwenda *Kinjeketile*. Jedwali na. 7 linaonesha tathmini ya usahili wa uhawilishaji huo.

**Jedwali Na. 7: Tathmini ya usahihi wa uhawilishaji wa viambishi viwakilishi vya jinsia katika *Kinjeketile***

| Na. | Kipashio Cha Kiswahili | Tafsiri Ya Kiingereza |
|---|---|---|
| **1.** | *A*liishi ngarambe (uk. v) | *He* lived at … (pg. v) |
| **2.** | *A*nataka … (uk. 12) | *She* is going … (pg. 12) |
| **3.** | *Ka*badilika sana (uk. 2) | *He's* changed (pg. 2) |
| **4.** | Sina cha ku*m*pa (uk. 1) | I have no food to give *him* (pg. 1) |
| **5.** | Nika*m*kuta mtoni (uk. 2) | I met *him* (pg. 2) |
| **6.** | … na mimi ni*m*saidie … (uk. 49) | … wants me to help *him* (pg. 53) |
| **7.** | Katazame *wa*napika nini (uk. 2) | Go see *she's* cooking (pg. 2) |
| **8.** | *Wa*natazama moshi … (uk. 4) | *She* looks at the smoke … (pg. 4) |

**Chanzo: Data ya maktabani (2025)**

Katika mfano Na. (1) na (2), kiambishi kiwakilishi *"a"* katika lugha chanzi kimehawilishwa na mfasiri kutumia kiwakilishi cha jinsia ya kiume *"he"* katika lugha lengwa.

"*A*metupa maji" – "*He* has given us water".

"Kwanini *u*natusaidia …" – "Why is *he* helping us"

Kulingana na muktadha, kiambishi kiwakilishi *"a"* katika mfano Na. (1) kinarejelea Kinjeketile ambaye anawakilishwa na kiwakilishi cha jinsia ya kiume "*he"* katika tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza na jinsia ya Kinjeketile ni wazi katika lugha chanzi. Hivyo, mfasiri anapotumia kiwakilishi cha jinsia ya kiume *"he"* katika lugha lengwa ni sahihi. Hata hivyo, matumizi ya kiwakilishi hicho hicho *"he"* katika lugha lengwa kuwakilisha mhusika Hongo ni tenge kwani, katika lugha chanzi, Hongo ni pepo na mwandishi hajadokeza jinsia ya Hongo kuwa ya kiume au kike katika lugha chanzi.

Aidha, katika mfano Na. (3) kiambishi *"ka"* kimetafsiriwa na mfasiri akatumia kiwakilishi cha jinsia ya kiume *"he"* katika tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza. Uhawilishaji wa kiambishi kiwakilishi *"ka"* katika lugha chanzi na kuwa *"he"* katika lugha lengwa, ni sahihi kwa kuwa, kiwakilishi *'he'* kinawakilisha Kinjeketile anayerejelewa na Bi. Kinjeketile na jinsia ya Kinjeketile ni wazi katika lugha chanzi. Isitoshe, mfano Na. (4), unabainisha kuwa, kiambishi kiwakilishi *"-m-"* kimehawilishwa na mfasiri akatumia kiwakilishi cha jinsia ya kiume *"him"* katika tafsiri ya Kiswahili kwenda Kiingereza.

"Sina cha ku*m*pa"

"I have no food to give *him*"

Uhawilishaji huu ni sahihi kwa kuwa kiwakilishi *"him"* katika lugha lengwa, kinawakilisha Kitunda ambaye jinsia yake ya kiume imebainishwa katika lugha chanzi.

Vilevile, mfano Na. (5) unaonesha kuwa kiambishi kiwakilishi *"wa-"* kimehawilishwa na kiwakilishi cha jinsia ya kike *"she"* kutumika katika tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza kulingana na kigezo hicho. Uhawilishaji wa kiwakilishi *"wa-"* katika lugha chanzi na kuwakilishwa na *"she"* kiwakilishi cha jinsia ya kike katika lugha lengwa, ni tenge kwani kulingana na muktadha, Bi. Kitunda anamtuma mtoto wake, akaangalie wanachopika wale waliokuwa kwenye nyumba ya Kinjeketile, lakini haijawekwa wazi nani aliyekuwa anapika; waliona tu moshi. Inabainika kwamba, mfasiri alichukulia kuwa, jinsia ya upishi kwa mujibu wa utamaduni wa Kiafrika ni ya kike kwa hivyo, akateua kiwakilishi cha jinsia ya kike katika tafsiri ya Kiswahili kwenda Kiingereza. Isitoshe, mfasiri amehawilisha meneno kamili kwa

misingi ya jininsia. Jedwali Na. 8 linaonesha tathmini ya usajili wa uhawilishaji huo.

**Jedwali Na. 8: Tathmini ya usahihi wa uhawilishaji wa viwakilishi (maneno) vya jinsia katika *Kinjeketile***

| Na. | Kipashio Cha Kiswahili | Tafsiri Ya Kiingereza |
|---|---|---|
| **1.** | Nyuma ya … alikuwa *jumbe* (uk. v) | Behind the was jumbe (*headman*) (pg. v) |
| **2.** | *Watu* … (uk. vi) | … *men* (pg. vi) |
| **3.** | *Bibi* Kitunda na *mtoto wake* (uk. 1) | A *mother* and *her daughter* (pg. 1) |
| **Na.** | **Kipashio Cha Kiswahili** | **Tafsiri Ya Kiingereza** |
| **4.** | *Mama* tazama (uk. 1) | Look *mother* (pg. 1) |
| **5.** | Shamba la *bwana* Kinoo (uk. 1) | *Bwana* Kinoo's plantation |
| **6.** | *Mtoto* wa Bi. Bolali amekufa (uk. 1) | Bibi Bolali *son* died … (pg. 1) |
| **7.** | *Wanaume* wenyewe wote … (uk. 2) | … alugha lengwa the *men* (pg. 2) |
| **8.** | Sina *babu* (uk. 2) | I don't have my *friend* |
| **9.** | *Mumewe* (uk. 3) | *Her husband* (pg. 3) |
| **10.** | … *udogo mwekundu* anatoa pesa … (uk. 7) | The *white man* pays welugha lengwa … (pg 8) |

**Chanzo: Data ya maktabani (2025)**

Uhawilishaji wa kiwakilishi *"headman"* katika lugha lengwa kutokana na neno *"Jumbe"* katika lugha chanzi kulingana na mfano Na. (1), kunadokeza jinsia ya mhusika jumbe kuwa ya kiume.

"Nyuma yake alikuwa *Jumbe* …"

"Behind the overseer there was *Jumbe (headman)"*

Uhawilishaji huu ni tenge kwa kuwa jinsia ya *"Jumbe"* katika lugha chanzi si wazi lakini katika tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza, mfasiri amebainisha jinsia ya Jumbe kuwa ya kiume kwa kutumia kiwakilishi *"headman"*. Katika mfano Na. (2), mwandishi ametumia neno *"watu"* katika lugha chanzi lakini mfasiri akawakilisha neno hilo katika lugha lengwa na kiwakilishi cha jinsia ya kiume *"men".*

*"Watu ..." – "... men"*

Uhawilishaji huu ni tenge kwa kuwa, katika lugha chanzi, mwandishi anasema, "*watu* wanaongea" lakini mfasiri katika lugha lengwa anasema *"the men relax ..."* Kiwakilishi *"men"* kinaashiria watu hao wote walikuwa wanaume jambo ambalo si wazi katika lugha chanzi.

European Journal of Linguistics
ISSN: 2957-4641 (online)
Vol. 4, Issue No. 2, pp 1 - 17, 2025
www.carijournals.org

Isitoshe, katika mfano Na. (3), mfasiri amehawilisha neno *"bibi"* na kutumia kiwakilishi cha jinsia ya kike *"mother"* katika tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza. Uhawilishaji huu ni sahihi kwa kuwa kulingana na muktadha *Bibi Kitunda*, anaandamana na mtoto wake hivyo mfasiri anapotumia kiwakilishi *"mother"* anarejelea *Bi Kitunda* na jinsia yake ya kike ni wazi katika lugha chanzi. Hali hii inajitokeza kabisa katika mfano Na. (4) ambapo mwandishi anasema *"mama tazama …"* na mfasiri katika lugha lengwa akasema, *"Look mother …"* ambapo neno *"mama"* katika lugha chanzi limetafsiriwa na kuwakilishwa na kiwakilishi cha jinsia ya kike *"mother"* katika lugha lengwa. Baada ya kutathmini usahili wa uhawilishaji wa viwakilishi vya jinsia katika vitabu teule mtafiti aliangazia asilimia ya uhawilishaji sahili na tenge katika kila kitabu teule. Jedwali Na. 9 linaonesha taarifa hizo.

**Jedwali Na. 9: Usahihi wa uhawilishaji wa viwakilishi vya jinsia katika vitabu vilivyotafsiriwa kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza**

| | **Uhawilishaji sahihi** | | **Uhawilishaji tenge** | |
|---|---|---|---|---|
| **Kitabu** | **Idadi** | **Asilimia** | **Idadi** | **Asilimia** |
| *Kaburi bila Msalaba* | 3/10 | 30 | 7/10 | 70 |
| *Siku Njema* | 18/22 | 82 | 4/22 | 18 |
| *Natala* | 13/15 | 87 | 2/15 | 13 |
| *Kinjeketile* | 9/23 | 38 | 14/23 | 61 |

**Chanzo: Data ya maktabani (2025)**

Uhawilishaji sahili na tenge kwa kuangazia vitabu vyote teule unaoneshwa katika jedwali na 10.

**Jedwali Na. 10: Usahihi wa uhawilishaji wa viwakilishi vya jinsia kijumla katika lugha lengwa**


| **Uhawilishaji sahihi** | | **Uhawilishaji tenge** | |
|---|---|---|---|
| **Idadi** | **Asilimia** | **Idadi** | **Asilimia** |
| 43/70 | 61 | 27/70 | 39 |

**Chanzo: Data ya maktabani (2025)**

Kwa kurejelea data katika Jedwali Na. 5.10 inabainika kuwa kati ya viwakilishi vya jinsia 70 vilivyohawilishwa kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza, asilimia 61 vilihawilishwa kwa usahihi lakini asilimia 39 ya uhawilishaji huo ukawa tenge.

Mchoro Na. 1 unaonesha uhawilishaji sahihi na tenge kwa jumla katika vitabu teule.

**Mchoro Na. 1: Usahihi wa uhawilishaji wa viwakilishi vya jinsia katika vitabu teule**




**Chanzo: Data ya maktabani (2025)**

Kwa kurejelea mchoro Na. 5.2, inabainika kuwa asilimia 61 ya uhawilishaji wa viwakilishi vya jinsia katika vitabu teule vilivyotafsiriwa kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza, ulikuwa sahihi ikilinganishwa na asilimia 39 ya uhawilishaji wa viwakilishi vya jinsia uliobainisha kuwa tenge.

**Hitimisho**

Uhawilishaji wa viwakilishi vya jinsia kutoka kiswahili lugha isiyo na viwakilishi bainifu vya jinsia kwenda kiingereza lugha yenye viwakilishi bainifu vya jinsia huwapa wafasiri changamoto nyingi kama ilivyodhihirika katika utafiti ambapo uhawilishaji wa viwakilishi huenda ukawa sahihi kulingana na muktadha au ukaazua utata na kuadhiri unjumbe asilia na hadhira lengwa. Matokeo ya uchunguzi wa usahihi wa uhawilishaji wa viwakilishi vya jinsia yamedhihirisha kuwa, katika riwaya ya *Siku Njema*, asilimia 82% ya viwakilishi vya jinsia vilivyohawilisha, katika tafsiri kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza vilihawilishwa kwa usahihi ikilinganishwa na asilimia 18% ya viwakilishi vilivyobainisha uhawilishaji tenge. Vilevile, katika riwaya ya *Kaburi bila Msalaba*, asilimia 30% ya viwakilishi vilihawilishwa kwa usahihi na asilimia 70% ya viwakilishi vikawa tenge katika kuhawilishwa kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza. Aidha, katika tamthilia ya *Kinjeketile*, asilimia 38% ya viwakilishi vilihawilishwa kwa usahihi lakini asilimia 62% uhawilishaji tenge. Katika tamthilia ya *Natala*, asilimia 87% ya uhawilishaji wa viwakilishi vya jinsia kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza,

ulikuwa sahihi lakini, asilimia 13% ya uhawilishaji ukawa tenge. Kwa jumla, asilimia 61% ya viwakilishi vya jinsia vilivyotafsiriwa kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza vilihawilishwa kwa usahihi ikilinganishwa na asilimia 39% vilivyokuwa tenge.

**Mapendekezo**

Katika ulimwengu wa tafsiri, mchakato wa uhawilishaji wa viwakilishi vya jinsia unachukua nafasi muhimu katika kuwasilisha ujumbe kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa. Tafsiri kutoka kiswahili kwenda kiingereza inakambiliwa na changamoto mingi ikiwa ni pamoja na jinsi viwakilishi vya jinsia vinavyoweza kuathiri uelewa wa ujumbe asilia. Utafiti huu umechunguza usahihi wa uhawilishaji wa viwakilishi vya jinsia hata hivyo, tafiti zaidi zaweza endelezwa kukuza na kuendeleza taaluma ya tafsiri kama vile kuchunguza athari za uhawilishaji wa viwakilishi vya jinsia kwa ujumbe ailia. Nafasi ya mtafsiri katika uhawilishaji wa viwakilishi vya jinsia katika tafsiri kutoka miktadha na tamaduni malimbali.

## MAREJELEO


Buljan, Gabrijela, Gradecak-Erdeljic, Tanja (2013). *English Morphosyntax on Nouns, Determiners and Pronouns*. Osijek: Filozofski fakultet.

Githiora, C. (2017) *An Unmarked Grave*: A Story of the Mau Mau War. Phonex Publishers.

Halliday, M. (2000). *An Introduction to Functional Grammer*. Beijing: Foreign Language Teaching and Research Press.

Hussein, E. (1970). *Kinjeketile*. Oxford University Press: Nairobi. (English).

Hussein, E. (1969). *Kinjeketile*. Oxford University Press: Nairobi. (Kiswahili).

Kareithi, P. (1969). *Kaburi bila Msalaba*: *Hadithi ya vita vya Mau Mau.* Nairobi: East African Publishing House.

Kasu, K. na Marami (2011). *Natala*. Nairobi. Marimba Publications Ltd.

Kennison, S. & Trofe, J. (2003). Comprehending Pronouns: A role for Word-specific Gender Stereotype Information. *Journal of Psycholinguistics Research*, 32: 355 – 378.

Khalilova, L. R. (2023). Lexical Gender in Written Business English: A Corpus-Based Approach. *Golden BRAIN*, *1*(4), 196–199. Retrieved from https://researchedu.org/index.php/goldenbrain/article/view/1630. Ilisomwa 15/11/2024

Khan, N. (2019). *Case Study as a Method of Qualitative Research in Qualitative Techniques for Workplace Data Analysis* (Kur. 170 – 196).

Kimutai, K. (2016). Ulinganifu wa Taarifa za Habari: Tathmini ya Tafsiri kutoka Kiswahili hadi Kipsigis katika kituo cha Kitwek. M.A Thesis University of Nairobi (Haijachapishwa).

Kweyu, D. na Kawegere, F. (2017). *A Good Day*. Longhorn Publishers.

Mberia, K. (1997). *Natala*. Nairobi. Marimba Publications Ltd.

Munday, J. (2001). *Introducing Translation Studies, Theories and Applications*. London: London and New York.

Ngesu, S., Malangwa, P. & Kandagor, M. (2019). "Tathmini ya Mikakati ya Tafsiri ya Vinay na Darbelnet (2004) katika tafsiri ya *A Good Day* (2019)." *Jarida la Mwanga wa Lugha*, Juz. 4(1): 129 – 152.

Nida, E. (1964). *Towards a Science of Translating: With Special Reference to Principles and Procedures Involved in Bible translating*. Leiden: Brill.

Riazi, A. (2018). "Mixed Methods Approaches to Studying Second Language Writing". *The TESOL Encyclopedia of English Language Teaching*, Juz. 10: 1-6.

Schaffner, C. (1988). *Skopos Theory*. In M. Baker (ed.) *Routledge Encyclopedia of Translation Studies*. London: Routledge, pp 235 – 238.

Venuti, L. (2000). *The Translation Studies Reader*. London and New York, Routledge.

Vermeer, H. (1989). *Skopos* and commission in translational action. In Chesterman, A. (ed.). *Readings in translation theory*. pp.173-187.

Walibora, K. (1996). *Siku Njema*. Nairobi: Longhorn.

©2025 by the Authors. This Article is an open access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution (CC BY) license (http://creativecommons.org/licenses/by/4.0/)